**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA**

**SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA**

**WILAYA YA UYUI**

**SHULE YA SEKONDARI IDETE,**

**S.L.P 640, TABORA.**

**TAREHE…………..…**

**MAWASILIANO**

**MKUU WA SHULE: 0782210747/0759031963**

**MAKAMU MKUU WA SHULE:**

**0767625565/0782403902. MATRON: 0652453639**

**BARUA PEPE: info@idete.sc.tz**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IDETE
S.L.P 640-TABORA

**MZAZI/MLEZI WA ………………………….……………………………………………..**
**S.L.P……………………………**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IDETE HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI MKOA WA TABORA MWAKA……………**

1. Ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao(Jina)**…………………………………………………………**
   Amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO (BWENI), tahasusi(combination) ya**…………..** katika shule hii kwa mwaka huu wa masomo………. Hivyo nachukua fursa hii kukupongeza sana wewe na mwanao.
2. Shule hii ipo mkoa wa Tabora kilomita 40 toka Tabora mjini barabara ya kuelekea Nzega Shule ipo Wilaya ya Uyui, Tarafa ya Uyui, Kata ya Isikizya, Ipo kilomita 4 toka Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Uyui mkabala na chuo cha VETA, usafiri upo wakati wote.
3. Anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………….Kwa ajili ya usajili tayari kuanza masomo Kwa muhula wa kwanza tarehe…………………….**.**
4. Mara upatapo barua hii na kuisoma kwa makini, tafadhali unatakiwa kumpatia mwanao mahitaji yote stahiki (yaliyoorodheshwa) ili kumwezesha afike shuleni mapema bila kupoteza muda wa masomo.

**5. SARE YA SHULE**

a) Sketi 2 rangi ya chocolate iliyoiva yenye rinda kubwa moja mbele na rinda kubwa

b) moja nyuma na marinda madogo mawili kwa kila upande (upande wa pembeni) Urefu

c) wa sketi ufike kwenye fundo mbili za miguu. b) Sweta 1 rangi ya chocolate iliyoiva

d) Shati 2 rangi nyeupe mikono mirefu na isiwe ya blue/blue bahari.

e) Sketi 1 rangi ya blue green yenye rinda kubwa moja mbele na rinda kubwa moja nyuma na marinda madogo mawili kwa kila upande (upande wa pembeni). Urefu wa sketi ufike kwenye fundo mbili za miguu (shamba dress)

f) Viatu vya ngozi jozi 2 nyeusi visivyofunga kamba. Bajaji haziruhusiwi. f) Soksi jozi 2 rangi nyeupe.

g) Viatu kwa ajili ya michezo (RABA). T-shirt ya rangi ya kijivu iliyoiva yenye kola kwa ajili ya kushindia isiyo na chapa yoyote.

h) Shuka jozi moja rangi ya blue.

i) Nguo za michezo ni track suit ya blue, T-shirt ya blue yenye kola isiyo na chapa yoyote.

j) Tai ya rangi ya chocolate iliyoiva (ifanane na sketi)

## 6. MAAGIZO MENGINE YA JUMLA KWA BWENI NA DARASANI

i. Godoro la sponji (6×21/2)
ii. Sanduku la chuma (Kuhifadhia Vifaa vyake).
iii. Mto mmoja na blanketi.
iv. Mswaki na dawa ya kutosha muhula mzima.
v. Sabuni ya kufulia na kuogea za kutosha muhula mzima.
vi. Vifaa vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko) visiwe vya plastic.
vii. Ndoo mbili (Plastic lita 10).zenye mfuniko
viii. Kwanja 1 (HGL), jembe 1 (HGL na PCB), reki 1 (PCB), mifagio 2, wa ndani na nje (HGL), mfagio 1 wa chooni na mopper 1(PCB).
ix. Fedha ya matumizi madogo madogo (Pocket money-ataitunza mwenyewe).
x. Jozi moja ya khanga au kitenge
xi. Aje na Ream mbili (2) ya karatasi (Size A4) kwa mwaka.
xii. Aje na madaftari Counter book (Quire 4) ya kutosha masomo yake.
xiii. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
xiv. Scientific Calculator;
xv. Aje na mathematical set, kalamu pamoja na calculator (Scientific) kwa wale wa masomo ya sayansi. (m)Ikipendeza mzazi anaweza kumnunulia mtoto wake vitabu vya masomo yake binafsi (Orodha ya vitabu imeambatanishwa). Aje na MOSQUITO NET kwa ajili ya kuzuia mbu.
xvi. Nguo za nyumbani pamoja na simu (aina yoyote) HAVIRUHUSIWI.
xvii. Nywele fupi- Hakuna kusuka wala kutia dawa.

## 7. MAAGIZO YA FEDHA

### A. MICHANGO MUHIMU

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

***Fedha za michango muhimu zote zilipwe benki yoyote Tanzania. ya NMBA/C Na:51001100143 NMB – IDETE SECONDARI***

**Ni marufuku mwanafunzi kufika shuleni na vitu vifuatavyo:-**

1. Nguo za nyumbani au kofia aina yoyote.

2. Vyakula vya aina yoyote mfano mkate, pipi, biskuti, sukari n.k

3. Vipodozi vya aina yoyote kama vile perfume, wanja, lipbam, rangi za kueha n.k

4. Redio, simu za mkononi, kamera n.k atakayebainika na vifaa hivi atafukuzwa shule

**MUHIMU KWA WOTE**

1. Kwa mawasiliano na rnwanao anapokuwa shuleni tumia narnba ya simu

**0769 586 396**
**0789 422 354**
**0659 892 393**
**0613 111 443**
} **PAUL JOHN MDAKI**

**Utaratibu wa matumizi**

**a.** Hizi ni simu za shuleni mahususi kwa ajili ya malezi ya watoto wanapokuwa shuleni kuwawezesha kuwasiliana na wazazi/walezi wao pale inapobidi.Hivyo basi hatutegemei mtoto kutumia simu nyingine yeyote kama hakuna ulazima huo au bila kibali rasmi.

b. Mwanafunzi atawasiliana na wazazi wake inapobidi kila mwisho wa wiki yaani Jumamosi na Jumapili kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 12:00 Jioni.Kumbuka simu hizi zinatumiwa na wanafunzi wote wanaokaa shuleni hivyo wazazi/Walezi mnaombwa kuwa makini siku hizo maana mtoto anaweza kukutafuta muda wowote kulingana na foleni yake inapomfikia.

c. Mtoto hatoruhusiwa kutumia/Kuongea na mzazi/mlezi siku za katikati ya wiki simu ikiwa hakuna dharura yoyote.Ikitokea dharura isiyohimilika au inayohitaji mzazi kufahamishwa,sisi walezi(walimu) tutaona busara

   i) Kukujulisha mzazi/mlezi

   ii)Kumruhusu mtoto kuongeana mzazi/Mlezi

d. Ikiwa nyumbani kuna dharura tunashauriwa mzazi asimjulishe mtoto kabla hajawasiliana na uongozi wa shule. simu za shule ziko wazi muda wote na siku zote za wiki.

e. Ikiwa nyumbani kuna dharura katikati ya wiki,simu za shule ziko wazi na mzazi anashauriwa kuwasiliana na uongozi wa shule kwanza ili kupata namna nzuri ya kushughulikia dharura hiyo bila kuleta taharuki au kuathiri maendeleo ya mtoto/mwanafunzi.

2. Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi unaruhusiwa kuja kumtembelea mwanao kwa siku itakayopangwa na uongozi wa shule arnbayo itakuwa ni mara moja kwa mwezi mzima jumamosi mwisho wa mwezi. Tafadhali usije na vyakula vya aina yoyote karna vile chips, maji, juisi n.k. Muda ni kuanzia saa 2 asubuhi hadi saa 10 jion.
3. Ni muhimu kumpatia mwanao fedha za kujikimu au fedha za matumizi binafsi kama matibabu na dharura nyinginezo awapo shuleni parnoja na nauli. Kumbuka hudhurio moja tu la kumwona daktari pale anapokuwa mgonjwa siyo chini ya Tshs.5000 /= bila dawa, Kama mwanao anavo kadi ya Bima ya Afya tafadhali aje navyo kwa unafuu wa matibabu yake akiwa shuleni.
4. Sare ya shule (sketi iwe ndefu mpaka chini kwenye enka ya mguu)
5. Mzazi/mlezi hakikish mwanao siwe na simu ya mkononi, (akikutwa na simu shuleni atafukuzwa na utatakiwa kulipa faini ya uharibifu wa miundo mbinu ya shule) na haturuhusu simu kuhifadhi shuleni au kwa mwalimu, matron, wapishi, walinzi au mfanyakazi yeyote au kwa watu mtaani au eneo lolote lile jirani na mzingira ya shule.

**SHERIA ZA SHULE**

Tabia njema (Heshima/Utii/ Adabu/Nidhamu/Ustaarabu/) ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni. Mwanafunzi mwenye tabia mbaya anaweza kukosa Elimu ya Sekondari au hata Elimu ya juu.Kila mwanafunzi anapaswa kufuata sheria/taratibu/kanuni zote za shule pia kuwatii Walimu,Watumishi wasio Walimu kuheshirniana na wanafunzi wenzake pamoja na waru wengine.

**A: SHERIA ZAJUMLA.**

1. Hairuhusiwi kunywa pornbe au kuvuta sigara/kiko au kutumia madawa ya kulevya ya aina yoyote ile.
2. Hairuhusiwi kuwa na mahusiano ya kimapenzi kati ya wanafunzi au mru veyote.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kuroka nje ya eneo la shule bila ruhusa kutoka kwa Mwalimu wa zarnu. Aidha Mtumishi yeyote wa shule akikuona mtaani/mjini au mahali popote ana haki ya kukutaka uonyeshe ruhusa.
4. Ruhusa ya kulala nje ya shule kwa sababu maalurn itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu wake tu.
5. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zitakazotolewa kulingana na utaratibu uliotolewa
6. Matusi ya aina yoyote ya kuandika au kutamka au kururnia ishara hayaruhusiwi.
7. Mwanafunzi unapaswa kujali na kutunza mali zako/shule/mtu yeyote, kwa mfano kutunza taa za umerne, miundo mbinu ya maji, kuepuka kuchora kwenye kuta, kwani uharibifu wowote utakaojitokeza kwa uzernbe wa mwanafunzi utaghararniwa na mwanafunzi mwenyewe.
8. Sare za shulet(uniforms) lazima zivaliwe wakati wa masorno na wakati wa kuruhusiwa kutoka nje ya shule.
9. Kila mwanafunzi ajiepushe na vitendo vya wizi wa mali za wanafunzi wenzake/mali za shule/mtu yeyote.
10. Kila mwanafunzi azingatie usafi wa mwili, mavazi, madarasa, mabweni, ukumbi wa chakula, na usafi wa maeneo ya shule kulingana na mgawanyo uliopangwa.
11. Kila mwanafunzi ajiepushe na vitendo vya ugomvi wa maneno au kupigana
12. Hairuhusiwi kuchelewa kufika shuleni wakati wa ukaguzi au kutoka likizo. Aidha mwanafunzi kama uliruhusiwa kwenda mjini au mtaani ni lazima kuzingatia muda wa kurudi ulioandikiwa kwenye ruhusa na ruhusa hiyo lazima irudishwe sehemu husika.
13. Mwanafunzi ni lazima kuonyesha tabia njema ukiwa ndani na nje ya shule kwani shule ina haki ya kukuadhibu ikiwa utaonyesha utovu wa nidharnu katika mazingira ya aina yoyote
14. Magazeti au picha zisizofaa hazitakiwi shuleni pia hairuhusiwi kuandika/kuchora ubaoni/ukutani.
15. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na tabia njema dhidi ya wanafunzi wenzake na watu wengine.

16. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyurnba ya Mturnishi yeyote bila ruhusa.
17. Hairuhusiwi kutumia bwenini vyombo vya umeme karna vile Pasi/Heater/Birika/Redio/Simu ua kufanya ufundi wa aina yoyote ile kwenye miundo mbinu ya umeme (bwenini au darasani).
18. Hairuhusiwi kuvaa kofia labda kuwe na sababu maalum zilizothibitishwa na daktari.
19. Kila mwanafunzi kwa vyovyote vile ni lazima kuhudhuria vipindi vya dini kulingana na Dini yake.
20. Kila mwanafunzi anapaswa kutii wito wa kengele kulingana na uraratibu wa shule
21. lkiwa kuna sababu maalurn ya mwanafunzi kuandika barua kwa idara moja wapo hapa shuleni, ni lazirna barua hiyo aandikiwe kwa Mkuu wa shule kupitia idara husika.
22. Kila mwanafunzi ni lazima awe na utii kwa Walimu na Watumishi wasio walimu au Wakuu wengine kwani ubishi na ujeuri wa aina yoyote hauruhusiwi kabisa.

**B: SHERIA ZA DARASANI**

1. Darasani ni mahali pa kujifunzia, kelele za aina yoyote haziruhusiwi. K.ila mwanafnzi anatakiwa kukaa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na mwalimu wa darasa
2. Mahudhuno darasani ni lazima kwa kiIa mwanafunzi wakati wa vipindi na mud a mwingine wa kujisomea ambao umepangwa na shule. Mwanafunzi mtoro atafukuzwa shule.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa kwenye meza au kiti cha mwalimu
4. Kila mwanafunzi ni lazima afanye usafi wa darasa kulingana na ratiba iliyopo.
5. Hairuhusiwi kufanya kikao chochote darasani bila ya ruhusa ya mwalimu wa darasa au mamlaka nyingine.

**C: SHERIA ZA BWENINI**

1. Bwenini ni mahali pa kulala na si mahali pakupiga kelele. Mazungumzo ya bwenini yawe ya maana na siyo matusi au lugha mbaya.
2. Haitakiwi kuwasha moto bwenini, Usafi wa bwenini ni wajibu wa kila mwanafunzi anaeyeishi bweni husika.
3. Hairuhusiwi kufanya vikao vya aina yoyote ile kwenye mabweni bila ruhusa ya mwalimu mlezi wa bweni.
4. Hauruhusiwa kulala bwenini wakati wa vipindi
5. Bweni hufungwa saa 1:15 asubuhi na kufunguliwa saa 10:40 jioni

**D. UTARATIBU WAADHABU.**

1. Mwanafunzi yeyote anayepewa adhabu lazima aifanve, ujeuri au ubishi wa aina yoyote utasababisha kuongezwa kwa adhabu hiyo. Kosa la kugomea adhabu linahesabiwa kuwa ni utovu wa nidharnu.
2. Mwalimu/Walimu watarnwadhibu mwanafunzi yeyote anayekiuka sheria/taratibu/kanuni za shule au sheria/taratibu/kanuni zitakazokuwa zimewekwa

na mwalimu wa zamu/mwalimu wa darasa/mwalimu mlezi wa bweni/mwalimu wa maeneo ya usafi ua mwalimu yeyote.

3. Mwanafunzi atapewa adhabu kulingana na kosa alilolifanya.
4. Mkuu wa shule anaweza kutoa adhabu kwa rnakosa makubwa kwa kumwadhibu mkosaji/kumsimamisha masomo kwa muda au kwa kupitia Bodi ya shule mwanafunzi anafukuzwa shule.

**E. TAHADHARI KWA WANAFUNIZI WOTE.**

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masorno bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu matusi kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na rntu yeyote yule.
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni. (wasichana hawaruhusiwi kusuka/kuweka dawa)
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pornbe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara, bangi.
x. Uasherati, uhusiano wa kimapenzitwa aina yoyote ile), kuoa au kuolewa.
xi. Kusababisha mimba, kupata rnirnba au kutoa mirnba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Uharibifu wa mali ya Umrna kwa makusudi.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe, nyumba za kulala wageni, parnoja na nyumba zawatumishi.
xv. Kumiliki, kukutwa au kuturnia simu ya mkononi katika mazingira ya shule. XV. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xvii. Udanganyifu wa mitihani ya ndani pamoja na kufeli mitihani,
xviii. Kubadili dini/dhehebu awapo shuleni pasipo kibali cha mzazi.

***Kwa taarifa zaidi kuhusu shule unaweza kutembelea tovuti ya shule ambayo ni: www.idete.sc.tz***

**NAKUTAKIA SAFARI NJEMA KUJA SHULENI IDETE SEKONDARI**

KARIBU SANA



**PAUL JOHN MDAKI**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IDETE
S.L.P 640-TABORA

**FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi

……………………………………………………………………………………………………
……

… Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi aitwaye

………………………………………………………………………..

………………………………… nimesoma na kuzielewa Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule na nimekubaliana nazo kama Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi na niko tayari kuzitekeleza sheria hizo pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

___________________

Mzazi/Mlezi wa

Mwanafunzi

**SHULE YA SEKONDARI**
**IDETE**

## A. FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili la Mwanafunzi ……………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………
3. Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………
4. Uhusiano na mlezi ……………………………………………………………………
5. Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi. Mkoa………….. Wilaya ……………………………...………Mtaa/Kijiji ………………………
6. Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………………
7. Kabila ………………………………….…. Dini ……………………………………………
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………
9. Wazazi wako hai au wamefariki (weka alama ya √)
   - Baba amefariki ( ) ●Baba yupo hai ( )
   - Mama amefariki ( ) ●Mama yupo hai ( )
10. Ndugu wengine wa karibu na Mzazi/Mlezi ambao wanaweza kutumika kama walezi wa mwanafunzi kama Mzazi/Mlezi husika hayupo

a) ………………………………………………….. mahali …………………………… b) ………………………………………………….. mahali …………………………… c) ………………………………………………….. mahali …………………………… d) ………………………………………………….. mahali ……………………………

**B. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi (Jina la Mwanafunzi)

…………………………………………………………………………………

Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na taratibu zote za shule ya bweni,na niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapokuwa shuleni hapa kama mwanafunzi. Nitakapokiuka kipengele chochote cha shule adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

…………………………………

………………………

Saini ya Mwanafunzi                                        Mkuu wa Shule

**PRIME MINISTER'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**UYUI DISTRICT COUNCIL**

IDETE SECONDARY
SCHOOL,
P.O. BOX
640,
TABORA

Date ……………………………

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

This form must be completed by Government Medical Officer

Student's full name :……………………………………………………………………..

Present age :…………………………………………………………………………

BloodTest :…………………………………………………………………………

Stool Examination :……………………………………………………………….

T.B.Test:………………………………………………………………………

Asthma:………………………………………………………………………

Eye Disorder :………………………………………………………………………

Nose Disorder:………………………………………………………………………

Ear Disorder:………………………………………………………………………

Anemia:……………………………………………………………………………

Chest:………………………………………………………………………………

Operations:…………………………………………………………………………

Serious Accidents:…………………………………………………………………….

Any other infections disease:……………………………………………………

Pregnancy:…………………………………………………………………………

Addition information e.g. physical defects or impairment, chronic or family diseases etc.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

I certify that I have personally examined Mr./Miss And found him/her fit unit to pursue studies

Signature ………………………………………………………….

Designation ………………………………………………………..

(Official stamp)

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI IDETE**

**MAAGIZO MUHIMU YA VITABU VYA KIADA NA ZIADA**

Ili mwanao aweze kupata ELIMU BORA Na kufikia kiwango kinachotakiwa na shule anapaswa kuwa na vitabu. Ifuatayo ni orodha ya baadhi tu vitabu ambavyo anapaswa kuja navyo ili aweze kumudu sawasawa mchepuo wake. ORODHA YA VITABU vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Kila mwanafunzi anatakiwa kununua baadhi ya vitabu hivyo kwa kila somo kwa masomo aliyopangiwa yaani HKL (History, Kiswahili na English Language) na PCB (Physics, Chemistry na Biology) General Studies ni kwa wote.

1. **KISWAHILI**

**1.1KISWAHILI 1**

Nadhariaya lugha ya Kiswahili

i. kidato cha tano na cha sita – Nyambari Nyangwine na masebo (2010)
ii. sarufi na fasihi sekondari na vyuo – Felician Nkwera
iii. sarufi na maumbo ya kiswahili sanifu (SAMAKISA): Sekondari na vyuo- kihore, Y. M. na masamba, D.P.B:TUKI (2003)
iv. Sarufi miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na vyuo – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B:TUKI(2003)
v. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI
vi. Tafsiri na ukalimani – Wanjara
vii. Kiswahili Sekondari – Taasisis ya Elimu

**1.2 FASIHI**

i. Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita – Masebo – Oxford University Press
ii. Nadharia na Tahakiki: Kiswahili 2 Saluhaya, S
iii. Tahakiki VItabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangwine na Masebo
iv. Fasihi – F.E.MK Senkoro

a) **TAMTHILIA (Walau vitabu viwili)**

I. Kivuli Kinaishi – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press
II. Kwenye Ukingo wa THimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
III. Nguzo Mama – Penina Muhando(1982)
IV. Morani – Emanuel Mbogo (1993)

b) **RIWAYA (Walau vitabu viwili)**

I. Vuta nikuvute, 4th ed – Shafi A. Shafi (2009)
II. Kufikirika, 4th ed Shaban Robert- Mkuki na Nyota
III. Mfadhili- Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
IV. Usiku Utakapokwisha, 2nd ed- Mbunda Msokile 2007-Macmillan Aidan

**c) USHAIRI (Walau vitabu viwili)**

I. Kimbunga : toleo la tatu (3rd Ed) – Haji Gora Haji (1995) TUKI
II. Chungu Tamu – Theobald Mvungi
III. Mapenzi Bora – Shaman Robert – Mkuki na Nyota Publishers
IV. Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu- Macmillan Aidan

**2. HISTORY**

I. Mastering Advanced Level History Book I & II- Kato (2010)
II. Basic Themes in European: Advanced Level History Paper I & II – Ismail Ngobi (2012)
III. Major Events in African History Paper I – Fr. Jovitus F. Kamara
IV. Tumaini, S.C.K (2010) Contemporary Historical Events: Advanced Level HistoryOne, Dar es Salaam: Shgibitali & Sons Publishers.
V. Yassin S. Essentials in Advanced Level History Paper 2, Dar es Salaam

**3. ENGLISH LANGUAGE.**

I. Advanced Level English: a Practical guide – Nicholous Asheri
II. Advanced Level Literature an Essential Guide – Nicholous Asheri

NOVELS

I. A man of the people- Chinua Achebe
II. The Beautiful ones are not yet Born – Ayi Kwei Armah
III. His Excellence Head of State – Dan Safo

**4. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

I. Basic Applied Mathematics by Kiiza and Septine I Sillem
II. Advanced Mathematics by Shayo
III. Advanced Mathematics Book 1 and 2 by Backhouse
IV. Advanced Mathematics Chand's 1 and 2

**5. PHYSICS**

I. Principles of Physics – Rogers Mancaster
II. Principles of Physics – Nelkon and Parker
III. Principles of Physics – Tom Duncan
IV. Calculations for Advanced Level
V. University Physics, New Edition
VI. Jim Breithaupt, understanding Physics 2nd / 4th Edition

**6. CHEMISTRY**

I. Inorganic Chemistry Part A-J.S. Maro
II. Inorganic Chemistry Part B – J.S. Maro
III. Advanced Level Inorganic Chemistry Part I –
TIE IV. Advanced Level Inorganic Chemistry Part II
– TIE V. Conceptual Chemistry – S. Chand
VI. Organic Chemistry – A.Ahdullah et.al. A. Level and 1st Year Undergraduate

Students Vol. III Part A

VII. Organic Chemistry – A.Ahdullah et.al. A. Level and 1st Year Undergraduate
Students Vol. III Part B

VIII. New Understanding Chemistry – Ted Sham

**7. GENERAL STUDIES**

I. General Studies for Advanced Level Certificate, Form Five-Richard R.F Mbalase

II. General Studies, Supplementary Book for Advanced Level and Colleges, 2nd Edition- Konrad Adenaker Stiftung

III. Bigirwamungu, J. & Deogratius S.M (2002) Understanding Advanced Level General Studies: Advanced Level Secondary School

IV. Nyangwine, C.M, Bukagile G.R & Maluka S.O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level: general Studies Notes Form 5 & 6

**8. BIOLOGY**

I. Biological science,Cambridge university press 1997 3rd Edition

II. Functional approach by Mbv Robert

III. New Understanding Biology by Suzan toole

IV. Advance Biology Principles and Application by C J Clegg and Mackean

V. Advanced Biology by Michael Kent (2000). Oxford University Press. UK